

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

MKATABA WA UJENZI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 28 mwezi 02 2022
~~2020~~

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha MPANDA, S.L.P. 190,
MPANDA ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya
Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana
kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

THABITIHI ATHUMANI BWIMILA S.L.P. 190, MPANDA
(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundu") kwa upande mwingine

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya
CHUNYA;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za
nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya CHUNYA;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Fundu kwa ajili ya kazi ya
KUWEKA DARI MABENENI MAWILI (2) (WASICHANA NA)
WAVULANA

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundu nakala ya Michoro pamoja na Mchanganuo
wa vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vinayoonesha namna kazi itakavyofanyika;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 4,200,000/-, Fundu
atafanya kazi ya DARI kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.
Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

- (a) Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi
- (b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya Ufundi;
- (c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya Ufundi;
- (d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80:30% ya Gharama ya Ufundi;
- (e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya Ufundi;na
- (f) Baada ya kukamilika kwa "Muda wa matazamio":5% ya Gharama ya Ufundi.

4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUHIRISHA KAZI

- (a) Fundi atakabidhiwa eneo la tarehe 28 mwezi 02 2020-22, au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.
- (b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku 15' toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.
- (c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

5. WAJIBU WA FUNDI

Fundi atakuwa na wajibu ufuatao: -

- (a) Kujenga Kuweka dari na kukamilisha ujenzi kama inavyoonekana katika Michoro pamoja na Mchanganuo wa Vifaavya Ujenzi (*Schedule of materials*) sambamba na maelekezo ya Mwajiri;
- (b) Kumpatia Mwajiri ratiba ya kazi (*work programme*) ndani ya siku 7 tangu tarehe ya kusaini Mkataba huu ili kupata kibali cha Mwajiri.

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA
MPANDA

Jina: JOSHUA MAMBORE Saini: [Signature]

Wadhifa: MKUU WA CHUO Tarehe: 28/02/2022

Mbele ya (Shahidi)

Principal
Mpanda Vocational Training Centre
P.O. Box 180
Mpanda

Jina: ERASMUS ZUMBA Saini: [Signature]

Wadhifa: MWALIMU (S) Tarehe: 28/02/2022

IMESAINIWA NA FUNDI

Mbele ya

Jina: THABITHI AFHUMANI BWIMBA Saini: [Signature]

Wadhifa: FUNDI Tarehe: 28/02/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: YUDA JOSEPH Saini: [Signature]

Wadhifa: FUNDI Tarehe: 28/02/2022